

40

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

Anwani ya Simu: "AFYA", DODOMA
Simu Nambari +255 026 -2323267
Fax No.
(Barua zote ziandikwe kwa Katibu Mkuu)
Unapojibu tafadhali taja:



Chuo Kikuu cha Dodoma,
Kitivo cha Sanaa na Sayansi ya
Maendeleo ya Jamii,
Jengo Na. 11,
S.L.P. 743,
40478 DODOMA.

Kumb. Na. 46/308/012/40

01 Februari, 2018

Katibu Mkuu,
Ofisi ya Rais,
Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa,
Jengo la Mkapa,
2 Barabara ya Nane,
S.L.P. 1923,
DODOMA.

YAH: KAMPENI ZA KUKUSANYA DAMU NCHINI

Kichwa cha habari hapo juu cha husika

Napenda kukutaarifu kuwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia Mpango wa Taifa wa Damu Salama Tanzania itafanya kampeni za kukusanya damu kama ifuatavyo:-

- Tarehe 26 - 30/3/2018 - Kampeni ya Robo mwaka**
- Tarehe 04 - 14/6/2018 - Siku ya wachangia Damu Duniani**
- Tarehe 24 - 28/9/2018 - Kampeni ya Robo mwaka**
- Tarehe 17 - 21/12/2018 - Kampeni ya Robo mwaka**

Kampeni hizo tajwa zina lengo la kutoa Elimu, kuhamasisha Jamii kuchangia Damu kwa hiari na kuongeza makusanyo ya Damu Nchini.

Tafadhali vitaarifu vituo (30) vya Damu Salama vya mikoa yote na Halmashauri zote mia moja themanini na nne (184) zishiriki pamoja na vituo saba (7) vya Kanda vya Damu Salama kutoa Elimu na kuendesha zoezi la kukusanya Damu lenye lengo la kukusanya Chupa 15,000 Nchi nzima **kila kampeni ya robo mwaka** na chupa 25,000 kwa **kampeni ya maadhimisho ya Siku ya wachangia Damu Duniani.**

Mgawanyo wa lengo katika kampeni za robo mwaka ni kama ifuatavyo;

1. Timu za Halmashauri kila moja, chupa 100
2. Timu za Mikoa katika vituo vya Damu salama, chupa 100
3. Timu za Damu Salama vituo vya Kanda chupa 500

Mgawanyo wa lengo katika kampeni ya Maadhimisho ya siku ya wachangia Damu Duniani ni kama ifuatavyo;

1. Timu za Halmashauri kila moja, chupa 200
2. Timu za Mikoa katika vituo vya Damu salama, chupa 200
3. Timu za Damu Salama vituo vya Kanda chupa 800

Aidha, chupa za damu zitakazokusanywa zitasaidia kuokoa vifo vitokanavyo na uzazi, vifo vya watoto chini ya Umri wa miaka 5, Wahanga wa ajali na Magonjwa mengine kama saratani

Nashukuru kwa ushirikiano wako.

mpoki
Dkt. Mpoki M. Ulisubisya
KATIBU MKUU – AFYA